**MADA YA KWANZA: MABARAZA YA KATA KAMA CHOMBO CHA UTATUZI WA MIGOGORO.**

- **Utangulizi**
- Moja ya wajibu wa msingi wa serikali za mitaa kama ulivyoanishwa katika kifungu cha 113 (1) (a) cha **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 Rejeo la la 2002** ni:-
- ***"****Kudumisha na kuwezesha uendelezaji wa amani na utengamano na utawala bora katika eneo lake."*
- Katika kutekeleza wajibu huu muhimu, serikali imeanzisha mabaraza ya kata katika maeneo yote ya Halmashauri. Mabaraza ya kata yamweanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha **Sheria ya Mabaraza ya kata Sura 206 Rejeo la 2002.**
- Kwa mujibu wa sheria hiyo ya mabaraza ya kata, kila kata itakuwa na baraza moja la kata, lakini waziri wa Seruikali za Mitaa anaweza kuanzisha mabaraza ya kata mawili katika kata moja.
-
- **Wajibu wa mabaraza ya kata**
- Kuimarisha amani na utengamano katika eneo lake la kazi, kuhakikisha migogoro inatatuliwa kwa njia za mazungumzo na kukubaliana. Kwa hiyo, ni muhimu Sana mabaraza ya kata yahimize na kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo, ikishindikana ndipo nyingine za utatuzi ziweze kuchukuliwa.
- Kuendesha kesi za madai na jinai. Aina ya kesi zitakazoshughulikiwa na mabaraza ya kata zimeonyeshwa katika nyongeza ya sheria ya mabaraza ya kata.
- Kuendesha usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Wajibu huu unawekwa na Sheria ya Ndoa, Sura 29 Rejeo la 2002, kwamba baraza la kata kuwa kama bodi ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa.
- Kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo thamani yake haizidi Tshs. 3, 000, 000/=. Wajibu huu unawekwa na Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura 216 Rejeo la 200
- Kushughulikia sheria ndogo za Halmashauri na Vijiji (vilivyo ndani ya kata hiyo).
- Kufanya kazi kama yatakavyoruhusiwa na sheria nyingine yoyote itakayotungwa na Bunge.
- **Wajumbe wa baraza la kata**
- Wajumbe wa baraza la kata wanatakiwa wawe kama ifuatavyo:-
- Sheria ya mabaraza ya kata katika kifungu cha 4, imeweka idadi ya wajumbe kuwa wasiopungua wanne lakini wasizidi wanane akiwemo mwenyekiti.
- Sheria ya mahakama ya migogoro ya ardhi katika kifungu cha11, inaweka idadi ya wajumbe kuwa wasiopungua wanne lakini wasiozidi wanane, wajumbe wanawake wasipungue watatu.
- Sheria ya ndoa katika kifungucha 103, inaweka idadi ya wajumbe wa bodi ya usuluhishi wa ndoa (ambayo ndiyo baraza la kata) wasiwe chini ya watatu na wasizidi sita akiwemo mwenyekiti.
- **Mambo ya kuzingatia**
- Ili kutokwenda kinyume na sheria tatu hizo kama zilivyoanishwa hapo juu, ni vema kamati za maendeleo ya kata ambazo ndizo zimepewa jukumu la kuteua baraza lakata wafanye yafuatayo:-

- Wateue wajumbe wanawake wasiopungua watatu na idadi ya wajumbe wote iwe wanane.
- Wakati wa kuendesha shauri, mabaraza ya kata yaheshimu sheria kwa kufuata na kuheshimu idadi kama inavyotakiwa na sheria husika. Mfano:
- -Kama baraza la kata likikaa kama bodi ya usuluhishi wa mgogoro ya ndoa, litapaswa wajumbe wasizidi sita na pia wasipungue watatu akiwemo Mwenyekiti.
- -Kama baraza la kata likikaa kama baraza la usuluhishi wa mgogoro wa ardhi litatakiwa wajumbe wawe watatu mmoja wao akiwa mwanamke. Baraza la kata likikaa kama mahakama ya ardhi, wajumbe watatakiwa wasipungue wanne lakini wasizidi wanane na kati yao wajumbe wanawake wasipungue watatu.
- -Baraza likikaa chini ya sheria ya Mabaraza ya kata, wajumbe wasipungue wanne lakini wasizidiwanane bila kujali jinsia.

**Uteuzi na sifa za wajumbe wa baraza la kata**

- Baraza la kata linateuliwa na kamati ya maendeleo ya katakutoka miongoni mwa wakazi wa kata husika. Kamati ya maendeleo ya kata inatakiwa itumie njia yoyote inayoona inafaa kuwapata wajumbe wa kuunda baraza la kata.
- Sifa za wajumbe wa baraza la kata:-
- Asiwe mbunge
- Asiwe mjumbe wa kamati ya maendeleo ya kata
- Asiwe mjumbe wa serikali ya kijiji
- Asiwe mwanasheria au mtumishi wa idara ya mahakama
- Asiwe mtumishi wa serikali
- Asiwe na umri chini ya miaka 18
- Asiwe kichaa/mwehu
- Asiwe mtu ambaye amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la kukiuka maadili
- Asiwe mtu ambaye sui raia wa Tanzania

**Katibu wa baraza la kata na muda wa wajumbe kukaa madarakani**

- Katibu wa baraza anapendekezwa na baraza la kata na kuthibitshwa na Halmashauri, ingawa anatakiwa aajiriwe na Halmashauri baada ya kupendekezwa na kamati ya maendeleo ya kata. Sifa ya katibu ni kuwa awe anajua kusoma na kuandika vizuri. Katibu ndiye mwandishi wa baraza la kata , lakini haruhusiwi kupiga kura.
- Wajumbe wa baraza la kata wanadumu kwa miaka mitatu lakini wanaweza kuchaguliwa tena. Endapo mjumbe ataachishwa ujumbe kwa kosa la kukosa sifa kama ziivyoelezwa hapo juu na mjumbe mwingine akateuliwa kuziba nafasi hiyo, basi atatumika kwa muda uliokuwa umebaki lakini anaweza kuteuliwa tena.

- **MADA YA PILI: BARAZA LA KATA KAMA BODI YA USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDOA.**

**Uwezo wa baraza**

- Baraza litakalokuwa na uwezo wa kuendesha usuluhishi ni lile ambapo mume anaishi na kama mume anaishi nje ya nchi basi baraza lile ambapo mke anaishi. Baraza ambalo mgogoro wa umepelekwa litawataka wahusika katika mgogoro huo na wale linaloona yafaa kuhudhuria.
- Endapo mtu yeyote aliyetakiwa kuhudhuria mbele ya baraza hilo amekaidi, barazalitapeleka maombi kwenye mahakama ya mwanzo au ya wilaya ili wito (summons) utolewe kwa mtu huyo.

**Baraza kutoa hati**

- Endapo baraza litashindwa kusuluhisha mgogoro huo litatoa hati inayoonesha matokeo ya usuluhisho huo.

**Uwakilishi**

- Wakili haruhusiwi kumwakilisha yeyote, pia mtuyeyote haruhusiwi isipokuwa mwanafamilia kwa idhini ya baraza.

**Katazo**

- Hairuhusiwi mtu kupeleka maombi ya talaka katika mahakama bila kupeleka mgogoro huo kwenye baraza la usuluhishi wa ndoa na baraza liwe limetoa hati kuonesha kuwa limeshindwakutatua mgogoro huo. Isipokuwa sharti hili (la kupeleka kwenye baraza) halitatumika endapo:-
- Mwombaji anadai kuwa ametelekezwa na hajui aliko mwenza.
- Mujibu maombi anaishi nje ya Tanzania na hakuna uwezekano kuwa atarudi ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya kupokelewa maombi.
- Mujibu maombi ametakiwa kuhudhuria mbele ya baraza na kwa makusudi ameacha kuhudhuria.
- Mujibu maombi amefungwa maisha na amehukumiwa kifungo cha miaka mitano na kuendelea au amewekwa kizuizini chini ya sheria ya kizuzi sura ya 361 na amezuiliwa kwa muda unaozidi miezi sita.
- Mwombaji anadai kuwa mujibu maombi anaumwa ugonjwa wa akili usiopona.
- Mahakama itaridhika kuwa yapo mazingira ambayo yanafanya kupeleka mgogoro mbele ya baraza kutowezekana.

**NB:**

- Baraza la kata pia linapewa mamlaka ya kuwa bodi ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na sehemu ya III ya nyongeza ya sheria ya mabaraza ya kata sura ya 206 Rejeo la 2002.

## MADA YA TATU: BARAZA LA KATA KAMA MAHAKAMA YA ARDHI.

**Utangulizi**

- Kifungu cha 167 cha Sheria ya Ardhi sura ya 113, kifungu cha 62 (2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji sura 114 na kifungu cha 3(2) cha Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi Sura ya 216 Rejeo la 2002, vifungu hivi vinaweka vyombo vyenye uwezo wa kushughulikia migogoro ya ardhi kuwa ni:-
- Baraza la Ardhi la Kijiji
- Baraza la Kata
- Baraza la Ardhi la Wilaya
- Mahakama kuu ya Tanzania – kitengo cha Ardhi
- Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.
- Mahakama za mwanzo na wilaya na hakimu mkazi hazihusiki kushughulikia migogoro ya madai ya ardhi. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi.

**Uwezo na wajibu wa baraza la kata kusikiliza migogoro ya ardhi.**

- Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Mabaraza ya kata, kinatoa madaraka kwa baraza la kata kuwa mahakama ya kushughulikia migogoro ya Ardhi katika eneo lake. Wajibu mkuu wa baraza la kata ni kuimarisha amani na utengamano katika eneo lake kwa kusuluhisha pande zote za mgogoro na kufikia muafaka kwa mazungumzo kuhusiana na tatizo la ardhi lililotokea katika Eneo lake.
- Katika kutekeleza wajibu wake, baraza litatilia maanani:-
- Taratibu za kimila zilizopo zinazotawala usuluhishi
- Haki za msingi
- Taratibu zozote ambazo wajumbe wa baraza wamefundishwa.

**Baraza linaweza kufanya yafuatayo:-**

- **KUSULUHISHA.**

**Hatua za kufuata wakati wa kusuluhisha**

- Kujitahidi kusuluhisha
- Mwenyekiti wa baraza kuteua wajumbe watatu kati yao mmoja anatakiwa awe mwanamke, mmoja wao anakuwa ni kiongozi na anatakiwa kuitisha kikao hicho cha usuluhishi.
- Wajumbe wanazikutanisha pande zenye mgogoro ili kuzisuluhisha. Katika kufikia usuluhishi kiongozi anakuwa na kura ya uamuzi.
- Endapo suluhu imewezekana baraza linasajili/linaandika makubaliano.
- `

**KUENDESHA KESI**

- Endapo suluhu imeshindikana basi kiongozi wa usuluhishi atarudisha mgogoro huo kwa mwenyekiti wa baraza, ambaye naye anaitisha kikao cha baraza kamili ambalo sasa litakaa kama mahakama na kuendesha kesi na kasha kupatikana mshindi.
- Baraza la kata linapoendesha kesi limeruhusiwa:-
- Kutoa agizo la ardhi inayogombaniwa kurudishiwa mshindi
- Kuagiza mkataba uliopo kati ya wanaogombana utekelezwe
- Kuagiza kusimamishwa kwa utekelezwaji wa jambo lolote hadi hapo kesi itakapoamuliwa
- Kuamuru kulipwa kiasi kilichoombwaambacho hakizidi milioni tatu
- Kuamuru kulipwa fidia
- Kuamuru kurejeshewa gharama za kesi ambazo upande uloshinda umeingia katikas kuendesha jkesi.
- Kuamuru jambo lololteambalo katika utekelezaji wa haki limeonekana ni la lazima.
- Baraza linaweza kupanga jinsi na namna na muda ambao fidia na gharama hizo zinaweza kulipwa.
- Endapo upande ulioshindwa utaacha kutekeleza hukumu kama ilivyoamriwa na baraza, baraza la kata litapeleka uamuzi huo kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kwa ajili ya kusimamia utekelezaji.
- Wakili wa kujitegemea haruhusiwikwenda kwenye baraza la kata kumwakilisha mtu au watu au kikundi cha watu.
- Baraza laweza kuruhusu ndugu au mmoja wa wanafamilia kwa kuombwa na mmoja w upande unaohusika na mgogoro kuhudhuria na kumwakilisha.
- Kama mmoja katika mgogoro au wote ni Taasisi, basi itapaswa iwakilishwe na mmoja wa viongozi wake au wafanyakazi wake ilimradi asiwe wakili.

**Rufaa**

- Yeyote ambaye hatakuwa ameridhika na uamuzi wa baraza la kata anaruhusiwa kukata rufaa kwenye baraza la ardhi na nyumba la wilaya. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha sheria ya mahakama za migogoro ya ardhi.
- Rufaa katika baraza la ardhi na nyumba inatakiwa ikatwe ndani ya siku arobaini na tano kuanzia siku ya hukumu ilipotolewa. Baraza la ardhi na nyumba la wilaya linaweza kuruhusu rufaa ikatwe hata baada ya siku arobaini na tano kuisha ilimradi kuwepo na sababu inayokubalika iliyosababisha kuchelewa huko.
- Sheria ya mabaraza ya kata inatoa siku sitini (60) za kukata rufaa kwa malalamiko yanayoshughukikiwa na sheria hii moja kwa moja.

**MADA YA NNE: TARATIBU ZA KUENDESHA MASHAURI KATIKA MABARAZA YA KATA.**

**Jinsi ya kupokea malalamiko**.

- Kifungu cha 11 cha sheria ya mabaraza ya kata kiaweka taratibu za kupokea malalamiko kama ifuatavyo:-

- Mtu mwenye lalamiko aweza kupeleka lalamiko hilo kwa katibu wa baraza , Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri , Mwenyekiti wa serikali ya kijiji, Mwenyekiti wa kitongoji au balozi wea nyumba kumi.
- Lalamiko linaweza kuwa la maandishi au linaweza kutolewa kwa mdomo, lakini Yule anayelipokea anatakiwa kuliandika na na kasha kumtaka aliyeleta lalamiko kutia sahihi pamoja na aliyelipokea.
- Endapo aliyepokea lalamiko hilo si katibu wa baraza, basi ataliwasilisha kwa katibu wa baraza ambaye ataliingiza lalamiko hilo katika rejesta na kulipa namba.

**Aina ya malalamiko ambayo baraza linaruhusiwa kupokea**.

**Makosa ya jinai**

- Makosa ya jinai ambayo baraza la kata limeruhusiwa kuyasikiliza yameelezwa katika sehemu ya kwanza na ya pili ya nyongeza katika sheria ya mabaraza ya kata (ambayo yameambatanishwa na kitini hiki0. Kesi pia zinazotokana na kuvunja sheria ndogo za Halmashauri au kijiji.

**Madai**

- Malalamiko ambayo ni madai yameelezwa katika sehemu ya tatu ya nyongeza ya sheria ya mabaraza ya kata. Mfano wa madai ni:-
- Ugoni
- Upatanishi chini ya sheria ya ndoa
- Migogoro midogomidogo kama mahari, migogoro ya ardhi
- Mgogoro wowote ambao waziri wa sheria anaweza kwa agizo litakalochapishwa katika gazeti la serikali atautangaza kuruhusu usikilizwe na baraza.

**Migogoro ya ardhi**

- Migogoro ya ardhi ni mojawapo ya aina ya malalamiko yanayyojulikana kama madai. Sheria ya Mahakama ya migogoro ya ardhi imeteua baraza la kata kama mahakama ya kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo thamani yake haizidi Tshs. 3, 000, 000/=.

**Wito (summons**)

- Katibu wa baraza ndiye atakayetoa wito kwa pande zinazohusika katika mgogoro.
- Wito utaeleza tarehe, muda na mahali ambapo baraza litakaa.
- Baraza linaweza kutoa wito kwa mashahidi endapo litaombwa na upande husika, lakini gharama ya upeleka wito huo itakuwa ni juu ya huyo anayeliomba baraza.

**Kuhudhuria.**

- 
- Pande zinazogombana zitatakiwa (isipokuwa motto au mtu ambaye hawezi kujitetea mwenyewe kwa sababu ya kuzuiliwa na afya) kufika zenyewe mbele ya baraza.

- Endepo tarehe iliyopangwa malamikaji hatahudhuria bila sababu yoyote, baraza litafukuza lalamiko hilo. Lakini endapo baraza litaona kuwa zipo sababu zinazokubalika ambazo zimemfanya mlalamikaji asihudhurie, au endapo amehudhuria lakini mlalamikaji hajahudhuria, baraza litaahirishwa hadi siku nyingine itakayopangwa, na baraza litatoa taarifa kwa mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri juu ya uahirishaji huo.
- Endapo mlalamikaji au mlalamikiwa ni motto mwenye umri usiofika miaka 18 au ni motto ambaye kutokana na sababu maalum hawezin kujieleza au kujitetea mwenyewe, baraza litaruhusu ahudhurie akiongozana na na mzazi au mlezi au ndugu au rafiki ambaye kwa kufuata taratibu atamsaidia katika kuendesha shauri hilo.

**kuendesha shauri**

- Mashauri yote yatatakiwa yawe wazi kwa umma ilima uweze kusikiliza mashauri hayo yakiendeshwa, isipokuwa kama baraza litaona kuwa kuruhusu umma kusikiliza shauri itakuwa siyo vyema.
- Baraza litajipangia taratibu za kuendesha mashauri na halitatawaliwa na taratibu zozote za sheria ya ushahidi.
- Mjumbe yeyote wa baraza ambaye atakuwa na maslahi katika shauri atatakiwa kueleza, na haruhusiwi kushiriki katika kusikiliza shauri hilo.

**Taratibu za uendeshaji wa mashauri.**

- Mlalamikaji atakuwa wa kwanza kupewa nafasi ya kueleza lalamiko lake, na kama anao mashahidi katika eneo linaposikilizwa shauri watatakiwa waondoke wakae mbali ili wasisikie kinachoelezwa.
- Mlalamikaji akimaliza kujieleza, upande unaolalamikiwa utaruhusiwa kumhoji, baraza puia litaruhusiwa kuhoji.
- Kisha mlalamikaji ataruhusiwa kuita shahidi wake mmoja baada ya mwingine nao watahojiwa na upande unaolalamikiwa pamoja na baraza.
- Baada ya hapo, upande unaolalamikiwa utakaribishwa kutoa maelezo na ukimaliza upande unaolalamika utaruhusiwa kuhoji kasha baraza.
- Kisha mlalamikiwa ataruhusiwa kuita mashahidui wake mmoja baada ya mwingine nao watahojiwa na upande unaolalamika pamoja na baraza.
- Hairuhusiwi kwa wajumbe wa baraza au mtu yeyote anayehoji kutumia lugha kali, ya matusi, au dharau. Ni wajibu wa Baraza kutunza utulivu na amani wakati wote wa kuendesha shauri. Endapo utulivu utapotea kutokana na pande zenye kulalamikianakupandisha jazba; baraza linawezakuahirisha kwa muda shauri hiloili kuruhusu hasira kupungua kisha shauri litaendelea kusikilizwa. Ni wajibu wa baraza kuendesha shauri kwa busara na uadilifu bila upendeleo au woga.
- Endapo siku iliyopangwa kusikiliza shauri hilo, utoaji maelezo au ushahidi utakuwa haujakamilika, Baraza litaahirisha shauri hilo na kupanga siku nyingine.

**Hukumu.**

- Hukumu ni uamuzi wa mahakama au baraza ambao unatolewa baada ya kupima maelezo na ushahidi uliotilewa.

- Ni vema hukumu ikawa ya kuandikwa na isomwe mbele ya umma.
- Baraza litatakiwa kukutana na kuandaa hukumu kwa pamoja likitilia maanani maelezo ya kila mjumbe na kama wajumbe watavutana basi uamuzi utakuwa kwa kura na uamuzi wa wengi ndio utakaokuwa uamuzi wa baraza.
- Uamuzi huo wa baraza utaandikwa kwa ufasaha ukieleza chanzo cha mgogoro, ushahidi uliotolewa na jinsi ushahidi huo unavyothibitisha au usivyothibitisha kutokea au uhalali wa lalamiko hilo.
- Wajumbe wa Baraza wanaokubali wataweka sahihi zao na kasha wale ambao hawakubali kama wapo nao wataweka sahihi.

**Tuzo**

- Baada ya hukumu kusomwa, hukumu itatakiwa kutoa tuzo kwa mujibu wa sheria. Tuzo ziko za aina nyingi kama ifuatavyo:-

**Tuzo chini ya sheria ya mabaraza ya kata.**

- Vifungu vya 9 na 17 vya sheria ya mabaraza ya kata vinatoa tuzo kama ifuatavyo:-
- Upande uliosababisha hilo lalamiko litokee kutakiwa uombe msamaha
- Mkosaji asemwe mbele ya mkutano mkuu wa kijiji au kwenye mkutano wa kata
- Kulipa faini kama itakavyopangwa na Halmashauri ya Wilaya au chombo chochote cha kisheria.
- Kumlipa mlalamikaji kiasi anachokilalamikia
- Mkosaji kuamriwa kufanya kazi za kijamii kama atakavyopangiwa na baraza.
- Mkosaji kulipa fidia.
- Pande zilizokuwa na mgogoro kutakiwa kufanya jambo lolote ambalo linaashiria kupatana.
- Kifungo.

**Tuzo chini ya sheria ya ndoa.**

- Kwa mujibu wa kifungu cha 104 cha sheria ya nmdoa, tuzo zinazoweza kutolewa na baraza la kata (ambalo ni bodi ya usuluhishi wa ndoa) ni kama ifuatavyo:
- Kuwapatanisha wanandoa
- Kama kupatana kumeshindikana, basi baraza litatoa hati au cheti na mapendekezo kuhusu baraza linavyoona mwenendo wa ndoa na kupeleka mahakama ya mwanzo.

**Tuzo chini ya sheria ya Mahakama za migogoro ya ardhi.**

- Kifungu chab 16 (1) cha sheria ya mahakama za ardhi kinaweka tuzo kama ifuatavyo:-
- Kurudishiwa ardhi inayogombaniwa.
- Kuamuru kutekelezwa kwa makubaliano ambayio walikuwa wamekubaliana
- Kutoa amri ya zuio
- Kuamuru kiasi kiachodaiwa kulipwa
- Kuamuru kulipa gharama za kuendesha shauri hilo ambapo upande wenye halali umeingia.

- Kutoa amri nyingine yoyote ambayo itadhihirisha kuwa haki imetendeka.

IMEANDALIWA NA

- JOSHUA SANGA
- MWANASHERIA WA WILAYA
- MASASI
- 25/01/2018.